

**BENKI KUU YA TANZANIA**  
16 Barabara ya Jakaya Kikwete  
S. L. P. 2303  
40184 DODOMA  
**TANZANIA**

Simu: +255 22 223 3173

Barua Pepe: botcommunications@bot.go.tz



**BANK OF TANZANIA**  
16 Jakaya Kikwete Road  
P.O. Box 2303  
40184 DODOMA  
**TANZANIA**

Phone: +255 22 223 3173

Email: botcommunications@bot.go.tz

**04 Machi 2024**

## **TAARIFA KWA UMMA**

### **TAARIFA ZA KUWEPO KWA SARAFU YA AFRIKA MASHARIKI HAZINA UKWELI WOWOTE, ZIPUUZWE**

Benki Kuu ya Tanzania inapenda kuutaarifu umma kwamba taarifa inayosambaa kuhusu kuanzishwa kwa sarafu ya Afrika Mashariki hazina ukweli wowote na zinapaswa kupuuzwa.

Benki Kuu inapenda kuujulisha umma kwamba mchakato wa kuanzisha sarafu moja kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki unaendelea na unatarajiwa kukamilika mwaka 2031.

Katika kutimiza azma hii, nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zinaendelea kutekeleza hatua mbalimbali za kuanzisha sarafu moja ya Jumuiya hiyo.

Mchakato huo unahusisha kuoanisha sera ya fedha na kufikia vigezo vya mtangamano wa kiuchumi kulingana na makubaliano ya nchi wanachama.

Aidha, juhudhi zinaendelea kufanyika ili kuanzisha Taasisi ya Fedha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (*East African Monetary Institute*) ambayo kukamilika kwake kutapelekea kuanzishwa kwa Benki Kuu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki itakayokuwa na wajibu wa kutoa sarafu mpya.

**IDARA YA MAWASILIANO  
BENKI KUU YA TANZANIA**